# USIRUKE KARIBU SANA NA JUA



SIMULIZI YA HADITHI YA UGIRIKI WA KALE, PAMOJA NA MICHORO MIPYA KWA MTINDO WA SANAA YA UFINYANZI WA KALE.



MAKTABA.ORG

kwa **Maktaba.org**
na **Brighid McCarthy**

**Leseni**: Creative Commons Attribution **CC BY**
Uko huru kunakili, kuchapisha, kubadilisha na/au kuuza.
Isipokuwa: Jina na logo ya Maktaba.org na Creative Commons
**Michoro**: Public Domain
Sanaa ilitengenezwa na Akili Bandia (AI)

**Pakua** kitabu hiki **bila malipo**:
**www.maktaba.org/book/1850**

Jiunge na **jamii** ya **wasomaji**.
Mapendekezo ya vitabu kwako.
Jiandikishe upate **Methali ya Siku**!
**Jadili** vitabu na ona zaidi:

- Vitabu vya Picha
- Vitabu juu ya Methali
- Hadithi za Mythology & Folklore
- Vitabu juu ya Historia ya Kale

HAPO ZAMANI ZA KALE, IKARUS NA BABA YAKE DAEDALUS WALIFUNGWA



GEREZANI KATIKA KISIWA CHA CRETE, NA MFALME MBAYA, MINOS.



DAEDALUS ALIKUWA SEREMALA BINGWA WA ATHENS.



SIKU MOJA, AKITAZAMA NDEGE ANGANI, ALIPATA WAZO JIPYA....



KWA KUTUMIA NTA NA MANYOYA, YA NDEGE, DAEDALUS AKATENGENEZA MABAWA MANNE: MAWILI KWAKE NA MAWILI KWA MWANAKE, IKARUS.



DAEDALUS AKIFUNGA MABAWA YA IKARUS ILI WATOROKE, AKAMTAHADHARISHA KWA DHATI: "USIRUKE JUU SANA KARIBU NA JUA, WALA USIENDE CHINI SANA KARIBU NA BAHARI, MWANANGU, BALI NENDA KATIKATI NA NIFUATE."



# IKAFANYA KAZI!
# WALIRUKA ANGANI!



WAFUGAJI NA WAVUVI WA PWANI WALIWAONA IKARUS NA BABA YAKE KAMA MIUNGU...



# IKARUS AKARUKA JUU... ZAIDI... NA ZAIDI...



ALIZIDIWA NA FURAHA AKARUKA JUU SANA. ALISAHAU KABISA ONYO NA USHAURI WA BABAKE.



HADI ALIPOKARIBIA NA JUA.... NA JOTO LIKAANZA KUYEYUSHA NTA ILIYOSHIKA MABAWA YAKE.



MANYONYA YA NDEGE YALIANGUKA CHINI BAHARINI...



ALIJITAHIDI KUPIGA MABAWA YAKE ILI KURUKA JUU, LAKINI MANYOYA YALIENDLEA KUANGUKA HADI ALIPIGA TU MIKONO YA KAWAIDA.



IKARUS AKAANGUKA BAHARINI NA KUZAMA.



# DAEDALUS

ALILIA SANA



DAEDALUS ALIITA KISIWA CHA PALE "IKARIA" KAMA KUMBUKUMBU YA MTOTO WAKE. HADI YA LEO, BAHARI ALIPOZAMA IKARUS INAITWA "BAHARI YA IKARIA".




DON'T FLY
TOO CLOSE
TO THE SUN